# Uchaguzi 2015: Vyuo Vikuu wameamua, Sekondari bado hawajaamua

Posted By Elias Mhegera - August, 21st 2015 **(677) Views**

---



KWA jinsi upepo wa kisiasa unavyovuma mpaka sasa, inaelekea vijana wengi wa vyuo vikuu wameegemea upande wa unganiko la Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA), walau kwa vyuo vikuu vilivyopo jijini Dar es Salaam.

Hali hiyo ilidhihirika siku za Alhamisi na Ijumaa, ya Agosti 13 na 14, 2015, wakati ulipohitimishwa mjadala wa umuhimu wa vijana katika kupaza sauti zao na kuchagua viongozi bora katika uchaguzi mkuu ujao.

Mjadala huo muhimu uliandaliwa na Chama cha Walimu wa Somo la Uraia (CETA) kwa kushirikiana taasisi ya kimataifa kutoka nchini Ujerumani ya Konrad-Adenauer-Stiftung (KAS). Wawasilishaji wa mada katika mdahalo huo walikuwa ni Dk. Chalres Kitima na Humphrey Polepole, aliyekuwa mjumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, maarufu kama Tume ya Jaji Warioba. Akiwasilisha mada kuhusu uchaguzi huru na wa haki, Dk. Kitima alisema kuwa pamoja na kwamba uchaguzi mkuu humbatana na mambo mengi, jambo la msingi ni kuilida amani ya nchi ili isije ikatoweka.

Akizungmzia dhana nzima ya uchaguzi huru na wa haki Dk. Kitima alisema kwa muda mrefu Tanzania ilikuwa kimbilio la mataifa mbalimbali na kwamba ndiyo maana hata wapigania uhuru waliishi hapa, akadai wananchi wakilisahau hilo nchi inaweza kutumbukia katika machafuko makubwa.

"Amani na utulivu kama ilivyo demokrasia, ni matunda ya uwekezaji wa muda mrefu. Nashukuru kwamba katika chuo nilichokiongoza cha Mtakatifu Agustino (SAUT) Mwanza, hatimaye tulifanikiwa kutoa mwanafunzi akawa mbunge wakati akiendelea na masomo chuoni. Huyu ni Felix Mkosamali, aliyekuwa Mbunge wa Muhambwe, Kigoma," alidokeza.

Kutokana na hali hiyo, Dk. Kitima aliwashauri Watanzania akisema amani iliyopo nchini, imejengeka kwa muda mrefu kwa ushirikiano wa Mwalimu Julius Nyerere na viongozi wenzake, na kwamba kwa jitihada zao, walihakikisha hakuna udini wala ukabila katika Taifa hili.

Hata hivyo, kazi ya uwasilishaji mada haikuwa rahisi kwa Dk Kitima, hasa pale baadhi ya wanafunzi wa vyuo vikuu walipoanza kuishambulia Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) wakidai kwamba haiaminiki, huku wakidai kuwa wao hawaoni mantiki ya kukumbushwa uchaguzi huru na haki.

"Sisi tunayasoma mambo haya kila siku madarasani kwetu. Tunataka majibu kutoka kwa wawakilishi wa Tume ya Uchaguzi, wako wapi? Tunataka watueleze nini maana ya goli la mkono, nini maana ya ushindi ni lazima," *alihoji kwa hamasa kubwa mwanafunzi mmoja aliyejitambulisha kwa jina la Francis Ipyana kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*.

Vijana hao walidai wamekuwa wakikanganywa na NEC kwa sababu katika kila uchaguzi, imekuwa na kawaida kwa wanavyuo kujiandikisha katika eneo tofauti na mahali wanapopigia kura kiasi cha kuhisi kwamba huo ni mpango mahsusi wa NEC kutokana na wengi wao kuwa mashabiki wa vyama vya upinzani.

Akijibu hoja hiyo kwa niaba ya waandaji, Mkurugenzi wa CETA, Safari Minja, alisema kwamba walitoa mwaliko kwa wawakilishi wa NEC lakini kwa bahati mbaya hawakutokea katika kongamano hilo. Hata hivyo aliahidi kuyafikisha madai yao hayo kwa wahusika hao. Baada ya majibu hayo, ilikuwa ni zamu ya kijana Godwin Johnson aliyeibua vicheko ukumbini hapo pale aliposema kwamba hawezi kuzungumzia uchaguzi wa Tanzania bila kugusia Jeshi la Polisi.

“Mbona sioni mada inayozungumzia Jeshi la Polisi? Kwani wao hawana mchango katika ushindi wa CCM?” alihoji kijana huyo na kushangiliwa na wenzake.

Akijibu maswali yaliyoelekezwa kwake, Dk. Kitima alisema Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Ibara ya 21 (1) na (2) inatoa uhuru kwa kila Mtanzania kushiriki katika uchaguzi kwa namna atakavyoona inafaa ili-mradi havunji sheria katika kufanya hivyo. Alisema ni jukumu la NEC kuhakiskisha kwamba inafanya kazi zake vizuri katika namna ambayo haitaacha shaka.

Hata hivyo, mwanafunzi mwingine Jacquline Maisana kutoka Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), alidai kwamba wapo wanavyuo wanaorubuniwa katika kuamua wampigie kura nani, ingawa hakufafanua hao wanaorubuniwa ni wa kambi gani hasa kisiasa. Hali ilivyokuwa katika mijadala hiyo, ilionekana wazi kwamba wanafunzi wengi wa sekondari ambao watapiga kura kwa mara ya kwanza katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, bado hawajaamua wampigie kura nani katika ngazi ya urasi wakati kwa wenzao wa vyuo vikuu, wengi wao wanaonekana kushabikia vyama vya upinzani, hususan Umoja wa Katiba ya Wanachi (UKAWA).

Kiashiria kikubwa cha hali hiyo, ni pale aliyekuwa Mjumbe Tume ya Mabadiliko ya Katiba (TMK), Polepole aliposhambuliwa vikali na wanavyuo kutokana na kuonyesha msimamo wake katika mitandao ya kijamii akimuunga mkono mgombea urais kupitia CCM, Dk. John Magufuli.

“Hebu tueleze Polepole, hivi wewe bado ni mchambuzi huru au ni ‘mpiga debe’ wa CCM? Tumekusoma sana kwenye mitandao ya kijamii ukimshambulia mgombea wa UKAWA, Edward Lowassa. Je, unategemea tutakuamini tena katika kauli zako?” alilalama kwa kuhoji mmoja wa wanavyuo hao.

Akitoa utetezi wake juu ya hoja hiyo, Polepole alisema: “Ninayo haki ya kidemokrasia kuonyesha nina muunga mkono mgombea gani. Ninashangaa mnataka kunyakua haki yangu wakati mimi sijawashambulia ninyi kwa kumuunga mkono Lowassa”

Miongoni mwa mambo yaliyovuta hisia na kutawala mjadala huo, ni ile kauli ya ‘goli la mkono’ iliyowahi kutolewa na mmoja wa viogozi wa juu wa CCM, Nape Nnauye, ambaye ni Katibu wa NEC (Itikadi na Uenezi) pamoja na kauli ile ya ushindi ni lazima iliyowahi kutolewa pia na mmoja wa viogozi wa juu wa chama hicho.

Wengi wa wanafunzi hao wa vyuo vikuu, walidai kuwa kwa jinsi wanavyofahamu, goli la mkono ni uporaji wa kura, huku wakaahidi kwamba safari hii watakuwa macho katika kulinda kura zao. Katika kufurahisha ukumbi wa mjadala huo, baadhi ya vijana kutoka shule za sekondari na vyuo vikuu, waliimba nyimbo mbalimbali kwa ustadi mkubwa, zikiwemo nyimbo za kuhimiza suala zima la uzalendo kwa Taifa hili.



Elias Mhegera
Media & Information Officer - Tanzania Human Rights Defenders Coalition | Tel: +255 754 826 272 | Email: mhegera@gmail.com

Source: FikraPevu ; http://www.fikrapevu.com/uchaguzi-2015-vyuo-vikuu-wameamua-sekondari-bado-hawajaamua/